



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU RIPOTI ZA
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA
MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2019**

06 Aprili, 2020

YALIYOMO

SURA YA KWANZA	3
UTANGULIZI WA JUMLA	3
SURA YA PILI	5
MWENENDO WA HATI ZA UKAGUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO	5
SURA YA TATU	8
MATOKEO YA UKAGUZI WA SERIKALI KUU	8
SURA YA NNE	18
MATOKEO YA UKAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA	18
SURA YA TANO.....	25
MATOKEO YA UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA	25
SURA YA SITA	32
MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO	32
SURA YA SABA	34
MATOKEO YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO	34
SURA YA NANE.....	36
MATOKEO YA KAGUZI MAALUMU	36
SURA YA TISA	37
MATOKEO YA UKAGUZI WA UFANISI	37
SURA YA KUMI	40
HITIMISHO	40

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

Ndugu Waandishi wa habari,

Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kukutana mahali hapa leo. Pia, ninamshukuru Mh. Rais kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha kwake Ripoti za Ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2019 na kuwezesha ripoti hizo kuwasilishwa Bungeni kupitia Waziri husika kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (ilivyorekebisha mwaka 2005).

Hii inadhihirisha wazi namna Mh. Rais anavyoathamini majukumu ya Ofisi yangu kwenye suala la uwajibikaji na uwazi katika kusimamia rasilimali za watanzania.

Ndugu Waandishi wa habari,

Kwa mwaka wa fedha 2018/19 nilifanya kaguzi za aina mbalimbali na kutoa taarifa zilizowasilishwa bungeni leo tarehe 6 Aprili, 2020 kama ifuatavyo:

- (i) Ripoti ya Serikali Kuu;
- (ii) Ripoti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (iii) Ripoti ya Mashirika ya Umma;
- (iv) Ripoti ya Miradi ya Maendeleo;
- (v) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi;
- (vi) Ripoti ya Ukaguzi wa mifumo ya Tehama; na
- (vii) Ripoti 12 za ukaguzi wa ufanisi zinazohusu sekta mbalimbali kama zilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Ripoti za Ufanisi za Kisekta

Na.	Jina la Ripoti
1.	Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Makusanyo ya Mapato kutoka kwa Makampuni ya Simu
2.	Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Upatikanaji wa Umeme na Uhakika wa Utoaji Huduma za Umeme
3.	Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Shughuli za Manunuzi ya Umma
4.	Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Miradi ya Ujenzi wa Maghala na Vihenge vya Kutunzia Mazao
5.	Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Shughuli za Kinga na Chanjo
6.	Ukaguzi wa Ufanisi kwenye Ubora wa Shughuli za Ujenzi na Ukarabati wa Barabara za lami Mijini

Na.	Jina la Ripoti
7.	Ukaguzi wa Ufanisi katika Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa ya Mifugo
8.	Ukaguzi wa Ufanisi kwenye Utekelezaji wa Jitihada za Kitaifa za Kupambana na utakatishaji wa Fedha nchini
9.	Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Ukusanyaji Mapato toka vyanzo vya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa
10.	Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Utoaji Programu za Kuwajengea Uwezo Walimu - Kazini
11.	Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Upatikanaji usioridhisha wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi yenye ubora kwa Watanzania.
12.	Ripoti ya ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa ufanisi yaliyotolewa mwaka 2016

SURA YA PILI

MWENENDO WA HATI ZA UKAGUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO

2.1 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

Ndugu Waandishi wa habari,

Katika ukaguzi wa Hesabu niliufanya kwa Taasisi za Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Miradi ya Maendeleo na Vyama vya Siasa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2019 nimetoa jumla ya Hati 1,082 za Ukaguzi. Kati ya hizo, Hati zinazoridhisha ni 1,017 (sawa na asilimia 94); Hati zenye shaka ni 46 (sawa na asilimia 4.25); Hati zisizoridhisha ni 7 (sawa na asilimia 0.64); na Hati Mbaya ni 12 (sawa na asilimia 1.11). Jedwali Na. 2, Na. 3 na Na. 4 yanaonesha mchanganuo wa Hati hizo.

Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi wa Hesabu kwa mwaka 2018/19

Aina ya Ripoti	Jumla ya Hati	Hati zinazoridhisha	Hati zenye shaka	Hati zisizoridhisha	Hati mbaya
Serikali Kuu	275	250	23	2	0
Mamlaka ya Serikali za Mitaa	185	176	9	0	0
Mashirika ya Umma	148	147	0	1	0
Miradi ya Maendeleo	455	441	13	1	0
Vyama vya Siasa	19	3	1	3	12
Jumla	1082	1017	46	7	12
Asilimia	100%	94%	4.25%	0.64%	1.11%

Jedwali Na. 3: Taasisi zilizopata hati zisizoridhisha

Namba	Jina la Taasisi	Aina ya Hati
1.	Ubalizi wa Tanzania Addis Ababa	Hati Isiyoridhisha
2.	Kampuni ya STAMIGOLD	Hati Isiyoridhisha
3.	Tume ya Taifa ya Mpango wa Utumiaji Bora wa Ardhi	Hati Isiyoridhisha
4.	Mradi wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni	Hati Isiyoridhisha

Ndugu Waandishi wa habari,

Jedwali Na. 4 linabainisha vyama vya siasa vilivyopata Hati yenye shaka, Hati isiyoridhisha na Hati mbaya.

Jedwali Na. 4: Vyama vya Siasa vilivyopata hati yenye shaka, hati mbaya na hati isiyoridhisha

Namba	Jina la Chama cha Siasa	Aina ya Hati
1.	Alliance for Africa Farmers Party	Hati Mbaya
2.	African Democratic Alliance(ADA TADEA)	Hati Mbaya
3.	Chama cha Ukombozi wa Umma(CHAUMMA)	Hati Mbaya
4.	Demokrasia Makini	Hati Mbaya
5.	Democratic Party	Hati Mbaya
6.	National Reconstruction Alliance	Hati Mbaya
7.	Alliance for Democratic Change	Hati Mbaya
8.	Chama cha Sauti cha Umma(SAU)	Hati Mbaya
9.	United Democratic Party(UDP)	Hati Mbaya
10.	United People's Democrtatic Party	Hati Mbaya
11.	Tanzania Labour Party	Hati Mbaya
12.	Union for MultParty Democracy (UMD)	Hati Mbaya
13.	The National Convention for Construction and Reform - Mageuzi (NCCR-Mageuzi)	Hati Isiyoridhisha
14.	Civic United Front (CUF)	Hati Isiyoridhisha
15.	National League for Democracy(NLD)	Hati Isiyoridhisha
16.	Chama cha Kijamii (CCK)	Hati yenye Shaka

2.2 Tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa miaka iliyopita

Ndugu Waandishi wa habari,

Katika ukaguzi wangu wa mwaka huu, nilifanya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa miaka iliyopita; kati ya mapendekezo 266 yaliyotolewa miaka iliyopita, mapendekezo 82 sawa na asilimia 31 yametekelezwa kikamilifu, mapendekezo 95 sawa na asilimia 36 utekelezaji wake unaendelea. Aidha, mapendekezo 67 sawa na asilimia 25 utekelezaji wake haujaanza; na mapendekezo 22 sawa na asilimia 8 yamepitwa na wakati. Mchanganuo wa utekelezaji umeainishwa katika **Jedwali Na. 5**.

Jedwali Na. 5: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo kwa miaka iliyopita

Aina ya Ripoti	Idadi ya Mapendekezo	Utekelezaji umekamilika	Utekelezaji unaendelea	Utekelezaji haujaanza	Mapendekezo yaliyopitwa na wakati
Mamlaka ya Serikali za Mitaa	11	0	2	9	0
Mashirika ya Umma	175	74	56	38	7
Serikali Kuu	80	8	37	20	15
Jumla	266	82	95	67	22
Asilimia	100	31	36	25	8

Ndugu Waandishi wa habari,

Kwa ujumla hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa miaka iliyopita hairidhishi, kwani kati ya mapendekezo 266 yaliyotolewa, ni mapendekezo 82 sawa na asilimia 31 yametekelezwa kikamilifu.

Hata hivyo, ukilinganisha na mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018, kiwango cha utekelezaji kimeongezeka ambapo kati ya mapendekezo 350 yaliyotolewa miaka iliyopita, mapendekezo 80 sawa na asilimia 22.9 yalitekelezwa kikamilifu.

Tathmini inaonesha kuwa jitihada zaidi zinahitajika ili kutekeleza mapendekezo yote kwa ukamilifu.

SURA YA TATU

MATOKEO YA UKAGUZI WA SERIKALI KUU

Ndugu Waandishi wa habari,

Katika Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2019, nimebaini mambo yafuatayo:

3.1 Usimamizi wa mapato yatokanayo na kodi

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2019, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya kiasi cha Sh. trilioni 15.74 kati ya makisio ya Sh. trilioni 18.29 hivyo kutofikia malengo kwa kiasi cha Sh. trilioni 2.55 sawa na asilimia 14. Jumla hii ya makusanyo haihusishi Sh. bilioni 20.05 za vocha za misamaha ya kodi na fedha za marejesho ya kodi kutoka Hazina. Mapato halisi ya mwaka wa fedha 2018/19 (yakijumuisha vocha za misamaha na marejesho ya kodi) ni Sh. trilioni 15.76.

Ukilinganisha na makusanyo halisi ya mwaka uliopita (2017/18) ambayo ni Sh. trilioni 15.40 kuna ongezeko la Sh. bilioni 360 sawa na asilimia mbili.

Ndugu Waandishi wa habari,

Nimebaini maeneo yafuatayo yatakayosaidia katika kuongeza mapato ya Serikali ili kufikia malengo yaliyowekwa endapo yatafanyiwa kazi kwa haraka.

3.1.1 Kodi zinazosubiri maamuzi ya mamlaka za rufaa za kodi

Katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2019, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikuwa na mashauri ya kodi kwenye Mamlaka za Rufaa za Kodi ya kiasi cha Sh. trilioni 366.04. Hata hivyo, kiasi hiki kimepungua kwa asilimia 4.6 ikilinganishwa na mwaka uliopita (2017/18) ambapo kulikuwa na Mashauri ya kodi ya kiasi cha Sh. trilioni 382.71.

Suala hili lina athari katika kiwango cha kodi kinachokusanywa na TRA. **Jedwali Na.6** linatoa mchanganuo wa mashauri hayo.

Jedwali Na. 6: Mashauri ya kodi katika mamlaka mbalimbali za rufaa za kodi

Mamlaka ya rufaa ya kodi	2018/19 Sh. (trilioni)	2017/18 Sh. (trilioni)
Bodi ya Rufani za Kodi	363.98	382.00
Baraza la Rufani za Kodi	1.45	0.07
Mahakama ya Rufani	0.61	0.55
Jumla	366.04	382.62

Ndugu Waandishi wa habari,

3.1.2 Mapungufu katika kusimamia pingamizi za kodi

Mamlaka ya Mapato imekubali pingamizi za kodi zinazofikia Sh. bilioni 84.62 zilizowasilishwa na walipa kodi mbalimbali. Hata hivyo, pingamizi hizi huchelewa kufanyiwa kazi kinyume na “Utaratibu wa TRA wa Huduma kwa Mteja”. Ucheleweshwaji huu una madhara katika kufikia malengo ya makusanyo kwani kodi yenye thamani hiyo inakuwa haijalipwa mpaka uamuzi wa pingamizi hizo utolewe.

3.2 Usimamizi wa mapato yatokanayo na kodi

3.2.1 Kodi za forodha zilizokadiriwa kwenye mafuta yaliyoingizwa nchini lakini hazikulipwa Sh. milioni 124.70

Nilibaini kodi zilizokadiriwa za Sh. milioni 124.70 ambazo hazikulipwa na Makampuni ya Mafuta. Hali hii ilisababishwa na ufuatiliaji usioridhisha wa maafisa wa Malamka ya Mapato katika kukusanya kodi zilizokadiriwa ambazo hazijalipwa.

3.2.2 Kodi na ada za bandari ambazo hazikukusanywa Sh. bilioni 3.58

Nilibaini kiasi cha lita milioni 11.69 za mafuta yaliyoingizwa kwenye mfumo wa forodha wa TANCIS lakini hayakukadiriwa kodi. Hivyo, kodi husika ya Sh. bilioni 3.58 (inayojumuisha kodi na ada za bandari) hazikukusanywa na Mamlaka ya Mapato.

3.2.3 Kutokukusanya riba baada ya malipo ya kodi kuchelewesha Sh. bilioni 1.36

Nilibaini ucheleweshwaji wa malipo ya kodi za forodha zinazotozwa kwenye mafuta yaliyotumika nchini. Hata hivyo, hakuna ushahidi uliotolewa na Mamlaka kuthibitisha kama riba ya kiasi cha Sh. bilioni 1.36 ilikusanywa kutokana na ucheleweshwaji huo.

3.3 Mchanganuo wa Deni la Serikali

Ndugu Waandishi wa habari,

Deni la Serikali linajumuisha madeni ya Serikali Kuu na Taasisi zake. Pia, linajumuisha dhamana zilizotolewa na Serikali iwapo Taasisi iliyodhaminiwa itashindwa kulipa madeni yake.

Deni la Serikali kufikia tarehe 30 Juni, 2019 lilikuwa Sh. trilioni 53.11 ambapo deni la ndani lilikuwa Sh. trilioni 14.86 na deni la nje ni Sh. trilioni 38.24 ikiwa ni ongezeko la Sh. trilioni 2.18 sawa na asilimia nne (4) ikilinganishwa na deni la Sh. trilioni 50.93 lililoripotiwa tarehe 30 Juni, 2018. Ongezeko la deni limesababishwa na riba ya mikopo, mikopo halisi na kushuka kwa thamani ya Shilingi.

3.3.1 Uanzishwaji wa kamati ya minada ya dhamana za Serikali (GSAC)

Nilibaini kutoanzishwa kwa kamati ya minada ya dhamana za Serikali (GSAC) kinyume na sehemu ya 3.4 (ii) ya mpango wa minada ya dhamana za Serikali wa mwaka 2018/19. Ukosefu wa kamati (GSAC) unapelekea kukosekana kwa kumbukumbu za kitaasisi na marejeo ya maamuzi kwa baadaye kutokana na kutowekwa kumbukumbu za kiofisi za maamuzi ya minada.

3.4 Mapungufu katika malipo ya mafao kwa wastaafu

Ndugu Waandishi wa habari,

Ukaguzi wangu ulibaini yafuatayo:

3.4.1 Udhaifu katika ukokotoaji wa malipo ya mafao

Katika ukaguzi wangu nilibaini majalada 338 kati ya majalada 3,448 yaliyokuwa yamekokotolewa kimakosa, kati ya hayo, majalada 170 yalikuwa na zaidi ya kiwango stahiki kwa Sh. milioni 316.12 na majalada 168 yalikuwa na kiwango pungufu kwa Sh. milioni 433.57. Kutokana na udhaifu huo, Serikali ingepata hasara ya Sh. milioni 316.12 kutokana na kuzidishwa kwa mafao, pia wastaafu wangelipwa kiasi pungufu cha Sh. milioni 433.57.

3.5 Usimamizi wa rasilimali watu

Ndugu Waandishi wa habari,

Ukaguzi wangu wa rasilimali watu ulibaini yafuatayo:

3.5.1 Malipo kwa watumishi hewa Sh. milioni 196.13

Ukaguzi wa malipo ya mishahara niliufanya katika Jeshi la Polisi ulibaini kiasi cha Sh. milioni 196.13 kilicholipwa kwa watumishi 11 ambao walikwishafariki, kufukuzwa kazi au kustaafu kinyume na matakwa ya Kanuni ya 113 (3) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001.

3.6 Usimamizi wa manunuzi na mikataba

Ndugu Waandishi wa habari,

Katika mapitio ya taratibu za manunuzi na usimamizi wa mikataba kwenye Taasisi mbalimbali za Serikali nilibaini mambo yafuatayo:

3.6.1 Ununuzi wa Vifaa na huduma bila mikataba Sh. bilioni 5.46

Katika mwaka wa fedha 2018/19 nilibaini kuwa Taasisi tano (5) za Serikali Kuu zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh. bilioni 5.46 pasipokuwa na mikataba.

Jedwali Na. 7: Taasisi za Serikali Kuu zilizofanya ununuzi bila ya mikataba.

Fungu	Taasisi	Maelezo	Kiasi(Sh)
38	Jeshi la Wananchi wa Tanzania	Ununuzi wa Sare za Jeshi toka kwa Mzabuni 21 st Century Textiles Ltd	4,242,319,008
51	Wizara ya Mambo ya Ndani	Ununuzi wa nyaya za LAN	28,667,583
57	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa	Ununuzi wa gari, kuchimba visima pamoja na ununuzi wa vifaa vya Ofisini	245,462,862
57	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa	Ukarabati wa kazi za nje pamoja na tanki la maji Kambi ya Ngerengere	737,974,120
39	Jeshi la kujenga Taifa	Ujenzi wa viwanja vya kuchezea mpira Melena na Mgulani JKT	205,677,653
Jumla			5,460,101,227

3.6.2 Mapungufu katika ujenzi wa mahakama 16

Ukaguzi ulibaini Mahakama ya Tanzania ilifanya malipo ya awali kwa Mkandarasi ya kiasi cha Sh. bilioni 4.83 kwa ajili ya Mahakama zote 16 lakini

Mkandarasi alilipwa malipo ya ziada ya kiasi cha Sh. bilioni 1.54 kwa ajili ya vifaa kinyume na makubaliano ya Mkataba.

Pia, nilibaini kuwa ujenzi wa Mahakama nne zinazojengwa Bunda, Kilindi, Katavi na Lindi ambazo zililipiwa malipo ya awali ya Sh. bilioni 1.47 ulikuwa umesimama toka mwezi Septemba 2017.

3.6.3 Malipo ya ununuzi wa huduma na vifaa ambavyo havikupokelewa vyenye thamani ya Sh. milioni 587.65

Taasisi saba (7) za Serikali Kuu zilifanya ununuzi wa vifaa na huduma vyenye thamani ya Sh. milioni 587.65 vilivyoagizwa na kulipiwa ambavyo havikupokelewa kinyume na makubaliano ya mkataba.

Jedwali Na. 8: Vifaa na huduma zilizolipiwa lakini hazikupokelewa

Fungu	Taasisi	Maelezo	Kiasi (Sh)
02	Tume ya Utumishi ya Waalimu	Ununuzi wa pikipiki kupitia GPSA	16,427,250
14	Jeshi la Zima Moto na Uokoaji	Ununuzi wa samani za Ofisini	96,483,200
14	Jeshi la Zimamoto na Uokoaji	Ununuzi wa sare za Jeshi	113,575,000
42	Bunge la Tanzania	Mfumo wa TEHAMA wa Maktaba	216,000,000
93	Idara ya Uhamiaji	Ununuzi wa viti, meza, madawati na kabati.	98,706,800
85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	Ununuzi wa jenereta la Ofisini.	35,000,000
28	Jeshi la Polisi	Ununuzi wa vifaa vya nyumbani	11,460,500
Jumla			587,652,750

3.6.4 Mapungufu yaliyobainika katika Mkataba wa ukusanyaji mapato kwenye Viwanja vya Taifa na Uhuru

Ukaguzi wangu ulibaini kwamba Wizara ya Habari, Vijana na Michezo iliingia Mkataba na Selcom Paytech PLC kwa ajili ya kufunga mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato katika viwanja vya Taifa na Uhuru kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia tarehe 1/7/2018 hadi tarehe 30/6/2020 kwa gharama ya asilimia 4.45 ya mapato yanayotokana na michezo na maonesho.

Hata hivyo, Wizara iliingia mkataba huo bila kuzingatia ushauri uliotolewa na Serikali ukiagiza Wizara kutoingia mkataba na kampuni zilizoshiriki mchakato wa zabuni ikiwemo M/s Selecom Paytech PLC na M/s Maxcom Africa Ltd.

Pia, Wizara haina mtaalamu wa TEHAMA anayesimamia stakabadhi zinazouzwa kupitia mfumo huo wa kielektroniki ili kuweza kujiridhisha idadi ya watazamaji kwa kila tukio la michezo mbali na kutegemea ripoti za mzabuni. Hii inatoa mwanya wa kuripoti kiasi pungufu cha mapato yanayokusanywa katika kila tukio la michezo.

3.7 Usimamizi wa matumizi

Ndugu Waandishi wa habari,

Katika mapitio ya taarifa za matumizi ya fedha za umma nilibaini dosari mbalimbali katika udhibiti wa ndani kama ifuatavyo:

3.7.1 Dosari kwenye malipo yaliyofanywa na Jeshi la Polisi katika ujenzi wa majengo Sh. milioni 806.69

Katika kupitia malipo yaliyofanyika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 400, mabweni na vyumba vya madarasa, nilibaini dosari zifuatazo:

Jedwali Na. 9: Dosari kwenye malipo yaliyofanywa na Jeshi la Polisi

Na.	Maelezo ya Dosari	Kiasi (Sh.Milioni)
1.	Malipo kwa vibarua kabla ya manunuzi ya vifaa vya ujenzi.	355.2
2.	Malipo kwenye akaunti binafsi badala ya fundi mchundo aliyesaini mkataba kwa ajili ya ujenzi wa jengo la makao makuu ya Polisi Dodoma.	145.2
3.	Malipo ya zaidi kwa kulinganisha na kiwango kilichokubaliwa kwenye jedwali la mahitaji kama gharama za vibarua katika ujenzi wa nyumba 30 zilizoko Mmedeli Mashariki Dodoma.	92.64
4.	Malipo kwa ajili ya vibarua kujenga msingi, kuta na linta hata hivyo malipo husika hayakuwa sehemu ya jedwali la mahitaji	105
5.	Menejimenti ililipia tofali zenye ukubwa wa inchi 6 kwa Sh.1,800 lakini Mzabuni alipeleka tofali za inchi 5 zinazouzwa kwa Sh 1,300 hivyo kupelekea kulipa Zaidi.	54
6.	Bidhaa za ujenzi zilizolipwa lakini hazikuwepo eneo la ujenzi.	54.65
	Jumla	806.69

3.7.2 Matumizi yasiyo na nyaraka toshelezi Sh. bilioni 5.06

Taasisi 39 zilifanya malipo yanayofikia Sh. bilioni 5.06 bila kuwa na nyaraka toshelezi. Kutokuwepo kwa nyaraka hizi kumezuia mawanda ya Ukaguzi wangu katika kuthibitisha usahihi wa matumizi yaliyofanyika.

3.7.3 Matumizi yaliyolipwa zaidi Sh. milioni 459.20

Mapitio yangu ya malipo yaliyofanywa yalibaini kuwa Taasisi sita (6) zililipa Sh. milioni 459.20 kwa ajili ya kununua vitu na huduma mbalimbali kwa bei ambayo ni juu ya kiwango.

Jedwali Na. 10: Orodha ya Taasisi zenye malipo yaliyozidishwa

Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi(Sh)
40	Mahakama ya Tanzania	75,273,219.00
56	TAMISEMI	13,121,600.00
86	Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga	31,620,000.00
72	Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma	7,537,417.00
85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	45,630,113.87
49	Wizara ya Maji	286,016,222.00
Jumla		459,198,571.87

3.7.4 Malipo yaliyofanyika bila kudai risiti za kielektroniki Sh. Milioni 895.37

Nimebaini kuwa Sh. milioni 895.37 zililipwa kwa wazabuni mbalimbali bila kudai risiti za kielektroniki kama inavyotakiwa na kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya 2015.

Jedwali Na. 11: Orodha ya Taasisi ambazo hazikudai risiti za Kielektroniki

Na	Fungu	Taasisi	Kiasi(Sh)
1	1003	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki-Idara ya Zanzibar	21,684,389
2	2	Tume ya Huduma za Walimu	1,233,236
3	31	Ofisi ya Makamu wa Rais	89,892,492
4	93	Idara ya Huduma ya Uhamiaji	6,592,602
5	36	Sekretarieti ya Mkoa Katavi	3,808,122
6	55	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	26,199,319
7	37	Ofisi ya Waziri Mkuu	3,328,000
9	83	Sekretarieti ya Mkoa Shinyanga	117,534,986
10	40	Mahakama ya Tanzania	57,301,075
11	81	Sekretarieti ya Mkoa Mwanza	20,779,120
12	56	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	86,775,208
13	70	Sekretarieti ya Mkoa Arusha	92,294,962
14	86	Sekretarieti ya Mkoa Tanga	29,400,000
15	80	Sekretarieti ya Mkoa Mtwara	122,686,053
16	52	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Walemavu	101,227,721
17	72	Sekretarieti ya Mkoa Dodoma	3,694,600
18	71	Sekretarieti ya Mkoa Pwani	98,152,296
19	79	Sekretarieti ya Mkoa Morogoro	12,788,580
Jumla			895,372,761

3.7.5 Matumizi yasiyo na tija Sh.milioni 948.93

Taasisi nne (4) zilitumia Sh. Milioni 948.93 katika matumizi yasiyo na tija kama inavyoonekana hapa chini.

Jedwali Na. 12: Orodha ya Taasisi zenye matumizi yasiyo na tija

Fungu	Taasisi	Aina ya Matumizi	Kiasi (sh.)
2	Tume ya Huduma ya Walimu	Malipo ya kodi ya nyumba ambayo haitumiki	2,400,000
39	Jeshi la Kujenga Taifa	Gharama za kuchelewa kutoa magari bandarini	57,515,912.65
81	Sekretarieti ya Mkoa Mwanza	Malipo ya dhamana ambayo haikuwa sehemu ya masharti maalum ya mkataba	3,496,333
85	Sekretarieti ya Mkoa Tabora	Gharama za nyongeza zilizotokana na kusimamisha kazi ya ujenzi	41,914,448
5	Tume ya Taifa ya Umwagiliaji	Tozo za ziada zilizotokana na kuchelewa kutoa mizigo bandarini	843,604,583
Jumla			948,931,276.65

3.8 Mapungufu yaliyobainika kwenye kaguzi za Balozi za Tanzania nje ya nchi

3.8.1 Kodi kubwa za pango kwa ajili ya nyumba za makazi ya Balozi Sh. bilioni 1.02

Nimebaini kuwa Balozi za Tanzania nchi za Brazil, Algeria na Sweden zilitumia Sh. bilioni 1.02 kukodi nyumba za makazi, kiasi ambacho kingeweza kuepukika kwa kukarabati nyumba za makazi zilizochakaa.

Jedwali Na. 13: Orodha ya Balozi zinazolipa kodi kubwa za pango

Jina la Ubalozi	Kiasi(Sh.)
Ubalozi wa Tanzania Brazil	274,061,808
Ubalozi wa Tanzania Algeria	514,095,600
Ubalozi wa Tanzania Sweden	228,045,300
Jumla	1,016,202,708

3.8.2 Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi katika Balozi mbalimbali Sh. milioni 645.07

Balozi tano (5) zilifanya malipo yanayofikia Sh. milioni 645.07 ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi kinyume na kanuni ya 95 ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001.

Jedwali Na. 14: Orodha ya Balozi zenye malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi

Jina la Ubalozi	Kiasi(Sh)
Ubalozi wa Tanzania Tanzania Canada	202,761,351.00
Ubalozi wa Tanzania Burundi	288,473,810.00
Ubalozi wa Tanzania Urusi	126,990,386.00
Ubalozi wa Tanzania Sweden	16,260,585.66
Ubalozi wa Tanzania Japan	10,580,246.00
	645,066,378.66

3.8.3 Majengo yaliyotelekezwa, ukarabati usiokamilika na viwanja visivyoendelezwa katika balozi zetu nje ya nchi

- (i) Nilibaini Balozi 14 zina majengo yaliyotelekezwa kwa muda mrefu yanayohitaji ukarabati mkubwa ili kuendelea kutumika. Balozi hizo ni: Geneva, Nairobi, Kigali, Maputo, Bujumbura, Kinshasa, Stockholm, Lusaka, Khartoum, New York, Pretoria, Washington, Lilongwe, na Harare.
- (ii) Pia, nilibaini ubalozi wa Tanzania Maputo ulianza ukarabati ambao haukukamilika hivyo kupelekea mkandarasi kudai riba iliyofikia kiasi cha Dola za Marekani 507,542.05 kwa kutolipwa kwa wakati kwa kazi iliyokuwa imekamilika.
- (iii) Balozi nane zimepewa viwanja kwa ajili ya kujenga Ofisi na makazi ambavyo havijaendelezwa kwa muda mrefu. Mfano Mji wa Sucheon, Korea Kusini, ulitoa kiwanja chenye mita za mraba 2,000 kwa Serikali ya Tanzania na baadaye kuchukua mita za mraba 800 baada ya kushindwa kuziendeleza kwa muda mrefu.

3.9 Ukaguzi wa vyama vya siasa

3.9.1 Utoaji wa fedha wenye mashaka kwenye akaunti ya Benki ya Chama cha Wananchi (CUF) - Sh. milioni 416

Chama cha Wananchi (CUF) kilipokea ruzuku kutoka Serikalini ya kiasi cha Sh. milioni 369.38 mnamo tarehe 5 Januari, 2017. Nilibaini kuwa katika fedha hizo, chama kiliamisha Sh. milioni 300 kutoka kwenye akaunti ya Chama kwenda akaunti binafsi ya mwanachama mnamo tarehe 6 Januari, 2017 na kiasi cha Sh. milioni 69 kilitolewa kama fedha taslimu. Hata hivyo, nyaraka za matumizi ya fedha hizo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Pia, nilibaini kiasi kingine cha Sh. milioni 47 kilitolewa kwenye akaunti ya benki ya Chama pasipokuwa na idhini ya Katibu Mkuu wa Chama kama ilivyoelekezwa kwenye Kanuni za Fedha za Chama cha Wananchi (CUF).

3.9.2 Mkopo uliotolewa kwenye Kituo kimoja cha Redio na Chama cha Wananchi (CUF) Haujarejeshwa- Sh. 85,000,000

Bodi ya Wadhamini ya CUF ilitoa mkopo wa Sh. milioni 45 mnamo tarehe 3 Januari 2017 kwa kituo kimojawapo cha redio cha mkoa wa Tanga kwa makubaliano ya kurejesha kwa kipindi cha miaka mitatu mpaka tarehe 03 Januari 2020. Aidha, Chama kiliidhinisha na kutoa mkopo mwingine wa Sh. milioni 35 tarehe 16 Februari 2018 kwa kituo hicho hicho cha redio kwa makubaliano ya kulipa kwa kipindi cha miaka miwili mpaka tarehe 16 Februari 2020. Pia, mkopo mwingine wa Sh. milioni 5 ulitolewa kwa kituo hicho tarehe 28 Mei 2019 wenye masharti ya urejeshwaji kwa kipindi cha siku 10 kuanzia tarehe ya kutoa mkopo.

Hata hivyo, mikopo yote haikuwa na dhamana; na hadi kufikia mwezi Januari 2020 wakati wa ukaguzi, kiasi chote cha Sh. milioni 85 hakikuwa kimerejeshwa. Aidha, nilibaini kuwa katika makubaliano ya mikopo hiyo, kituo hicho cha redio kiliwakilishwa na wakurugenzi wake watatu (3) ambao pia ni wakurugenzi wa CUF. Katika mazingira haya, upo mgongano mkubwa wa kimaslahi kwenye makubaliano yaliyofanyika.

3.9.3 Matumizi yasiyokuwa na Tija ya Kumfidia Mpangaji bila kufuata utaratibu - Sh. Milioni 60

Nilibaini kuwa Jumuiya ya Wazazi (CCM) ilimuondoa mpangaji bila kufuata taratibu. Matokeo yake, mpangaji alionesha nia ya kufungua kesi ya madai ya kulipwa fidia ya Sh. milioni 800. Hata hivyo, Jumuiya ya Wazazi ililipa kiasi cha Sh. milioni 60 kama fidia ya hasara baada ya kufanya mazungumzo nje ya mahakama na suala hilo kumalizika.

SURA YA NNE

MATOKEO YA UKAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA

Ndugu Waandishi wa habari,

Nilifanya ukaguzi katika Mamlaka 185 za Serikali za Mitaa. Katika ukaguzi huo nilibaini masuala mbalimbali ambayo Serikali inapaswa kuyafanyia kazi ili kuboresha usimamizi wa rasilimali za umma. Yafuatayo ni baadhi ya mambo yaliyojitokeza katika Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa:

4.1 Usimamizi wa maandalizi na utekelezaji wa bajeti

4.1.1 Makusanyo pungufu yatokanayo na vyanzo vya ndani Sh. bilioni 121.46

Katika mwaka wa fedha 2018/19, Mamlaka 126 za Serikali za Mitaa zilipanga kukusanya mapato ya jumla ya Sh. bilioni 463.95 kutokana na vyanzo vya ndani, mamlaka hizo zilifanikiwa kukusanya Sh. bilioni 342.49 hivyo kuwa na upungufu wa Sh. bilioni 121.46 sawa na asilimia 26 ya bajeti yote.

4.1.2 Bakaa ya Sh. bilioni 258.66 za ruzuku ya miradi ya maendeleo

Katika mwaka wa fedha 2018/19, Mamlaka 182 za Serikali za mitaa zilipokea jumla ya ruzuku ya maendeleo Sh. bilioni 913.69. Hata hivyo, fedha zilizotumika ni Sh. bilioni 655.03 na kubaki na jumla ya Sh. bilioni 258.66 sawa na asilimia 28 ya fedha zilizopokelewa.

Kushindwa kutumia fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati kunakwamisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi kama ilivyokusudiwa.

4.1.3 Sh. bilioni 17.41 za mapato ya vyanzo vya ndani hazikupelekwa kwenye Miradi ya Maendeleo

Ukaguzi ulibaini kuwa kiasi cha Sh. bilioni 109.44 kilikusanywa na Mamlaka 60 za Serikali za Mitaa ambapo kati ya kiasi hicho, Sh. bilioni 43.78 kilipaswa kutengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwa ni asilimia 40 mpaka 60 ili kutekeleza matakwa ya Sehemu ya 5.0 (xiii) ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/19.

Hata hivyo, kiasi cha Sh. bilioni 26.37 tu ndicho kiliamishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na kuacha kiasi cha Sh. bilioni 17.41 ambacho hakikupelekwa.

4.1.4 Matukio yanayoashiria ubadhirifu katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

Wakati wa ukaguzi, nilibaini matukio ya udanganyifu yenye jumla ya Sh. bilioni 1.25 ambayo yanahitaji uchunguzi zaidi. Matukio haya yanaashiria mapungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani inayolenga kubaini na kudhibiti vitendo vya udanganyifu. Matukio haya yameoneshwa katika **Jedwali Na. 16**.

Jedwali Na. 15: Matukio ya udanganyifu

Na.	Halmashauri	Aina ya udanganyifu au ubadhirifu	Kiasi (Sh.)
1.	Wilaya ya Itigi	Fedha taslimu zilizokosekana katika Ofisi ya fedha	6,376,000
2.	Manispaa ya Kondo	Fedha ambazo hazijaenda benki	16,185,760
3.	Wilaya ya Iramba	Makusanyo ambayo yalikabidhiwa kwa Mweka Hazina lakini hayakuwasilishwa benki.	117,540,845
4.	Manispaa ya Songea	Makusanyo yaliyooneshwa katika daftari la mapato kutoka mfumo wa makusanyo lakini hayakuonekana katika taarifa ya benki	81,252,264
5.	Manispaa ya Songea	Makusanyo ambayo hayajawasilishwa benki yaliyoonyeshwa katika daftari la mapato kutoka mfumo wa makusanyo kwa kutumia stakabadhi za kughushi.	50,512,264
6.	Wilaya ya Madaba	Makusanyo yaliyoonyeshwa katika daftari la mapato kutoka mfumo wa makusanyo kuwa yamewasilishwa benki lakini hayakuonekana katika taarifa ya benki.	124,687,887
7.	Wilaya ya Kyela	Makusanyo ambayo hayajawasilishwa benki na wakala aliyeachishwa kazi tangu tarehe 30 Agosti, 2018.mwenye namba ya utambulisho 303900005877	14,475,000
8.	Manispaa ya Moshi	Karatasi saba za leseni zilizonyofolewa kutoka katika vitabu vya leseni. Karatasi zilizonyofolewa ni 2654123, 2654129, 2654165, 2655320, 2655321, 2655360 na 2655466.	0
9.	Wilaya ya Siha	Makusanyo yaliyofanyika kwa kutumia stakabadhi za kuandika kwa mkono (HW5) ambayo hayajawasilishwa benki.	282,878,934
10.	Wilaya ya Tabora	Makusanyo ya mapato yaliyotumika kabla ya kuwasilishwa benki	31,846,000
11.	Wilaya ya Kibondo	Shughuli zilizotekelezwa bila kupata idhini ya Afisa Masuuli.	479,728,396
12.	Wilaya ya Kibondo	Malipo yaliyokiuka utaratibu wa mgawanyo wa majukumu.	41,915,720
		Jumla	1,247,399,070

4.2 Usimamizi wa Mishahara na rasilimali watu

4.2.1 Malipo ya mishahara kwa watumishi waliokoma utumishi wao Sh. milioni 167.44

Ukaguzi ulibaini malipo yaliyolipwa kwa watumishi waliokoma utumishi wao ya kiasi cha Sh. milioni 167.44 kutokana na sababu mbalimbali kama vile kustaafu, kufariki, utoro kazini au waliofukuzwa kazi.

Kati ya kiasi kilicholipwa, Sh. milioni 132.66 ilikuwa ni malipo ya mishahara na Sh. milioni 34.77 ikiwa ni makato ya watumishi hao.

Jedwali Na. 16: Makato na malipo ya mishahara kwa watumishi waliokoma utumishi wao

Na.	Halmashauri	Jumla ya kiasi kilicholipwa (Sh.)
1.	Manispaa ya Arusha	4,131,000
2.	Wilaya ya Buchosa	14,942,000
3.	Wilaya ya Handeni	1,235,000
4.	Manispaa Ilemela	5,514,000
5.	Wilaya ya Kondo	1,716,000
6.	Wilaya ya Korogwe	13,506,284
7.	Wilaya ya Kwimba	1,235,000
8.	Wilaya ya Madaba	4,530,000
9.	Wilaya ya Misungwi	8,824,172
10.	Wilaya ya Muheza	2,015,752
11.	Wilaya ya Ngorongoro	7,597,000
12.	Wilaya ya Rombo	5,486,000
13.	Wilaya ya Sengerema	9,164,000
14.	Wilaya ya Siha	84,633,000
15.	Wilaya ya Simanjiro	2,906,000
Total		167,435,208

Sababu kubwa ya kutokea kwa mapungufu hayo ni pamoja na kutohuishwa kwa wakati taarifa za watumishi katika mfumo na mawasiliano hafifu kati ya Mamlaka na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Hazina kwa ajili ya kufuta watumishi ambao hawapo tena katika utumishi wa umma.

4.3 Tathmini ya Miradi inayotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Ndugu Waandishi wa habari,

Ukaguzi ulibaini mambo yafuatayo:

4.3.1 Miradi ambayo haikutekelezwa Sh. bilioni 25.97

Nilibaini Mamlaka 19 za Serikali za Mitaa zilishindwa kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopangwa yenye thamani ya Sh. bilioni 24.70 kutokana na kutokuletwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu na makusanyo hafifu ya mapato ya ndani.

Vilevile, kazi za miradi zenye thamani ya Sh. bilioni 1.27 katika halmashauri 12 hazikutekelezwa licha ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo zilikuwepo.

4.3.2 Miradi ambayo haikukamilika Sh. bilioni 77.51

Nimebaini miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 77.51 ambayo haijakamilika katika Mamlaka 81 za Serikali za Mitaa iliyosababishwa na ucheleweshaji wa fedha, ushiriki hafifu wa jamii kwenye shughuli za maendeleo, usimamizi usioridhisha na baadhi ya miradi kutelekezwa kwa muda mrefu.

4.3.3 Miradi iliyokamilika lakini haitumiki Sh. bilioni 12.66

Nilibaini uwepo wa miradi 42 yenye thamani ya Sh. bilioni 12.66 kwenye Mamlaka 33 za Serikali za Mitaa iliyokamilika lakini haitumiki. Kutokana na hali hiyo, thamani ya fedha kwa miradi hiyo haikufikiwa.

4.3.4 Fedha za utekelezaji wa miradi zilitumika kwenye shughuli zisizokusudiwa Sh. bilioni 1.25

Nilibaini Mamlaka 13 za Serikali za Mitaa zilichepusha fedha za miradi ya maendeleo jumla ya Sh. bilioni 1.25 na kuzitumia kwenye shughuli ambazo hazikukusudiwa kinyume na Kifungu cha 43 (5) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka, 1982. Hii inamaanisha kuwa shughuli zilizokusudiwa hazikufanyika jambo linaloweza kuathiri malengo ya halmashauri husika katika kutoa huduma bora kwa jamii.

4.4 Manunuzi na usimamizi wa mikataba

4.4.1 Manunuzi ya bidhaa na huduma yasiyoshindanishwa Sh. bilioni 32.46

Nilibaini jumla ya Sh. bilioni 32.46 zililipwa na Mamlaka 74 za Serikali za Mitaa kwa ajili ya gharama za ujenzi, huduma na bidhaa bila kushindanisha wazabuni,

kinyume na Kanuni ya 131(5), 159 na 164 za Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 (kama zilivyorekebishwa mwaka 2016). Hali hii inaweza kupelekea gharama kubwa ya manunuzi kutokana na kukosa ushindani.

4.4.2 Manunuzi ya Sh. bilioni 9.23 yalifanyika bila idhini ya bodi za zabuni

Nilibaini Mamlaka 47 za Serikali za Mitaa zilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma yenye thamani ya Sh. bilioni 9.23 bila kupata idhini ya bodi za zabuni kinyume na Kanuni za 55(2), 163(4) na 185(1) za Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (kama zilivyorekebishwa mwaka 2016).

4.4.3 Bidhaa zilizopokelewa bila kukaguliwa na kamati za ukaguzi na mapokezi Sh. bilioni 5.01

Nilibaini Mamlaka 43 za Serikali za Mitaa zilipokea bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 5.01 bila kukaguliwa na kamati za ukaguzi na mapokezi kinyume na Kanuni za 244 na 245 za Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (kama zilivyorekebishwa mwaka 2016).

4.4.4 Bidhaa za Sh. bilioni 1.09 zililipiwa lakini hazikupokelewa

Nilibaini kuwa mamlaka 27 za Serikali za Mitaa ziliagiza na kulipia bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 1.09 ambazo hazikupokelewa. Kiasi hiki kinajumuisha Sh. milioni 619.15 zilizolipwa na Hazina kwa Bohari Kuu ya Madawa kwa ajili ya vifaa vya upasuaji ambavyo havijapokelewa katika vituo vya afya vilivyokarabatiwa.

4.4.5 Nyongeza ya Sh. bilioni 1.22 kwenye mikataba isiyoidhinishwa na Bodi za Zabuni.

Nilibaini Mamlaka 9 za Serikali za Mitaa zilikubali kutoa nyongeza kwa mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 1.22 bila kupata idhini ya Bodi za Zabuni katika halmashauri husika. Hii ni kinyume na Kanuni ya 110(5) na (6) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013.

4.4.6 Sh. bilioni 3.58 zililipwa kwa wakandarasi bila tathmini ya kazi kufanyika

Nilibaini Mamlaka tano za Serikali za Mitaa zilifanya malipo ya kiasi cha Sh. bilioni 3.58 kwa wakandarasi na mafundi bila kuthibitisha ukubwa wa kazi zilizofanyika kinyume na Kanuni ya 243 (2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (kama zilivyorekebishwa mwaka 2016).

4.5 Usimamizi wa matumizi

4.5.1 Malipo yaliyofanyika bila kuwa na viambatisho vinavyojitosheleza Sh. bilioni 3.45

Nilibaini matumizi yenye jumla ya Sh. bilioni 3.45 kwenye Mamlaka 92 za Serikali za Mitaa hayakuwa na viambatisho vinavyojitosheleza. Kwa kukosekana kwa viambatisho hivyo, nilishindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

4.5.2 Malipo kwa bidhaa ambazo hazikupokelewa Sh. milioni 452.74

Nilibaini malipo yenye jumla ya Sh. milioni 452.74 yalifanyika kwenye Mamlaka tisa za Serikali za Mitaa kwa ajili ya bidhaa na huduma ambazo hazikupokelewa.

4.6 Usimamizi wa mapato

4.6.1 Mapungufu katika Sera ya ukusanyaji wa ushuru wa huduma

Nilibaini Mamlaka 18 za Serikali za Mitaa hazikukusanya ushuru wa huduma kutoka katika makampuni 2,242 yanayoendesha shughuli zake katika maeneo husika ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kutokukusanywa kwa ushuru wa huduma kutoka kwa makampuni husababisha ukosefu wa mapato ambayo Mamlaka za Serikali za Mitaa zingetumia katika kuboresha utoaji wa huduma katika jamii husika.

Pia, nilibaini kuwa Mamlaka 58 za Serikali za Mitaa zilikusanya mapato ya jumla ya Sh. bilioni 5.84 yanayohusu ushuru wa huduma bila uthibitisho wa taarifa za mapato kutoka kwa makampuni husika ili kuhalalisha kiasi kilichokusanywa.

4.6.2 Mashine za kukusanyia mapato za kielektroniki (POS Mashine) hazikusajiliwa katika mfumo wa taarifa wa ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRCIS)

Ukaguzi wa Mfumo wa ukusanyaji wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRCIS) ulibaini mashine 14 za kukusanyia mapato za kielektroniki (POS machine) ambazo hazikusajiliwa wala kuonekana katika Mfumo wa taarifa wa Ukusanyaji wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRCIS). Kitendo hiki kinatoa mwanya wa upotevu wa mapato na kusababisha Halmashauri kushindwa kufikia malengo yake.

4.6.3 Marekebisho ya ankara za wateja katika mfumo wa mapato (LGRCIS) yaliyofanywa na kuidhinishwa na mtu mmoja katika mfumo wa LGRCIS

Nilibaini marekebisho ya ankara katika Mamlaka 19 za Serikali za Mitaa yenye thamani ya Sh. milioni 626.65 yaliyofanywa na kuidhinishwa na mtu mmoja kinyume na aya ya 10 ya maagizo yaliyotolewa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

Kukosekana kwa mgawanyo madhubuti wa majukumu katika uombaji na uidhinishaji wa marekebisho ya ankara ya mapato kwenye mfumo kunaweza kupelekea upotevu wa mapato kwa watu wasio waaminifu.

4.6.4 Marekebisho katika Mfumo wa Kukusanyia Mapato (LGRCIS) bila uwapo wa nyaraka za kuthibitisha marekebisho hayo yenye thamani ya Sh. bilioni 3.32

Nilikagua marekebisho ya mapato yaliyofanyika katika mfumo wa kukusanyia mapato na kubaini marekebisho yenye thamani ya Sh. bilioni 3.32 kwenye Mamlaka 12 za Serikali za Mitaa bila kuwapo kwa maelezo sahihi kwa nini marekebisho hayo yamefanyika. Pia, marekebisho hayakuambatanishwa na nyaraka zinazothibitisha uhalali wa marekebisho hayo.

Marekebisho yanayofanywa bila kuwa na nyaraka za kuthibitisha marekebisho hayo huweza kusababisha Halmashauri kupoteza mapato yaliyokusanywa bila Menejimenti kugundua.

4.6.5 Maduhuli yaliyokusanywa bila ya uthibitisho wa kupelekwa Benki Sh. bilioni 10.39

Nilibaini kiasi cha Sh. bilioni 10.39 kilichokusanywa katika Mamlaka 84 za Serikali za Mitaa hakikuthibitishwa kupelekwa benki kinyume na Agizo la 50 (5) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa la mwaka 2009.

Kutokana na kukosekana kwa taarifa za kupeleka maduhuli benki, sikuweza kuthibitisha uhalali, usahihi na ukamilifu wa kiasi cha mapato ya ndani kilichokusanywa na kuripotiwa katika taarifa za hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika.

4.6.6 Maduhuli yaliyokusanywa na mawakala lakini hayakuwasilishwa Halmashauri Sh. bilioni 2.27

Nilibaini maduhuli yaliyokusanywa katika Mamlaka 16 za Serikali za Mitaa na Mawakala kiasi cha Sh. bilioni 2.27 hayakuwasilishwa Halmashauri kwa ajili ya kupelekwa benki. Hii inapelekea upotevu wa mapato kwa Halmashauri husika.

SURA YA TANO

MATOKEO YA UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA

5.1 Kaguzi za Mashirika ya Umma ambazo hazikuhitimishwa

Hadi kufikia tarehe 1 Machi, 2020 nimefanikiwa kuhitimisha na kutoa hati za ukaguzi kwa mashirika 148 (78.3%) kati ya mashirika 189 niliyoyakagua. Hati za Ukaguzi kwa mashirika 41 kati ya 189 hazikutolewa kwa sababu mbalimbali kama kuchelewa kuitisha vikao vya Bodi za Wakurugenzi vya kuridhia hesabu kwa wakati na ucheleweshwaji wa majibu ya hoja za ukaguzi. Mashirika ambayo hayakuwasilisha hesabu ili zitolewe Hati ya Ukaguzi zinaonyeshwa katika Jedwali Na. 18.

Jedwali Na. 17: Mashirika ambayo hayakuwasilisha hesabu zake kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali Taasisi ambazo hazijawasilisha hesabu zake kutokana na sababu mbalimbali

Na.	Shirika
1	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Bariadi
2	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania
3	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Geita
4	Chuo cha Uhasibu Arusha
5	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga
6	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Karatu
7	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Korogwe
8	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Kyela
9	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Makambako
10	Kampuni ya Huduma za Meli
11	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Mpanda
12	Taasisi ya Mifupa Muhimbili
13	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Muleba
14	Chuo kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere
15	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Namtumbo
16	Taasisi ya Tija ya Taifa (NIP)
17	Shirika la Bima la Taifa (NIC)
18	Makumbusho ya Taifa Tanzania
19	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Ngara
20	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Njombe
21	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Nzega
22	Procurement and Supplies Professional and Technicians Board (PSPTB)
23	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga/Rukwa
24	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Same
25	Sharing World
26	STAMICO

Na.	Shirika
27	TCA CCC
28	Bodi ya Maziwa Tanzania
29	Kampuni ya Mbolea Tanzania
30	Tasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)
31	Mamlaka ya Usimamizi ya Bima Nchini (TIRA)
32	Benki ya Uwekezaji wa Maendeleo Tanzania (TIB- DEV)
33	Bodi ya Nyama Tanzania
34	Baraza la Taifa la Blashara Tanzania
35	Shirika la Reli la Tanzania (TRC)
36	Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania
37	Shirika la Magazeti Tanzania (TSN)
38	Shirika la Simu Tanzania (TTCL)
39	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Tukuyu
40	UTT-AMIS/PID
41	Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundistadi (VETA)

5.2 Kutohibitishwa kwa lita bilioni 1.4 za Bidhaa za Petroli kwa ajili ya matumizi ya ndani

Katika kupitia ripoti ya utendaji kwa bidhaa za petroli zilizoingizwa nchini kwa kipindi cha kati ya Mwaka wa Fedha 2015/16 na 2018/19, nilibaini lita zipatazo bilioni 9.9 za bidhaa za petroli ziliingizwa nchini lakini bidhaa za petroli zilizothibitishwa kwa matumizi ya ndani zilikuwa lita bilioni 8.5 na hivyo kuwa na tofauti ya lita bilioni 1.4 kati ya bidhaa za petroli zilizothibitishwa na bidhaa za petroli zote zilizoingia nchini kwa matumizi ya ndani. Pia, nilibaini kuwa Mamlaka ya Udhubiti wa Nishati na Maji (EWURA) haikuwa na utaratibu unaoiwezesha kubaini chanzo cha tofauti iliyoonekana.

Tofauti iliyoonekana inaashiria udhaifu katika ufuatiliaji wa bidhaa za petroli zilizoingia nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani, ambapo inaweza kusababisha upotevu wa mapato.

5.3 Taasisi zenye wadaiwa sugu Sh. bilioni 224.69

Nilibaini kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma yana fedha nyingi ambazo zinashikiliwa na wadaiwa sugu. Kati ya Mashirika 148 ambayo nimeyakagua, nilibaini uwepo wa Mashirika 34 yenye wadaiwa sugu yanayofikia kiasi cha Sh. bilioni 224.69. Mengi katika madeni haya yanahusiana na mauzo ya huduma mbalimbali kwa wateja. Naamini madeni haya yanaweza kupunguzwa kwa kiasi kikubwa kama Taasisi zitakusanya mapato kupitia mfumo, kufuata mkakati wa malipo kabla ya huduma na kuongeza nguvu katika mbinu za kukusanya madeni.

Mfano wa Mashirika yenye wadaiwa sugu ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 19.

Jedwali Na. 18: Taasisi zenye wadaiwa sugu

Taasisi	Shs '000,000'
Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	83,520.00
Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi	65,698.28
Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania	54,392.22
Shirika la Nyumba la Taifa	11,679.53
Kampuni ya Ubungo Plaza	9,403.62
Jumla	224,693.65

5.4 Watoa huduma kutokuwasilisha taarifa za fedha za muda na malipo ya ushuru wa mwaka

Katika sampuli ya watoa huduma 16 kati ya 980 wenye leseni, nilibaini kulikuwa na watoa huduma watano ambao hawajawahi kulipa ushuru wala kuwasilisha taarifa za hesabu za muda wa robo mwaka kwa Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) kama taratibu zinavyotaka. Kiasi cha ushuru husika kinachokadiriwa kuwa Sh. bilioni 10.35 hakijakusanywa. Pia, nilibaini mtoa huduma mmoja kati ya hao 16 ambaye amekuwa akiwasilisha taarifa za fedha lakini hajawahi kulipa ushuru unaofikia kiasi cha Sh. milioni 502.44.

5.5 Kuongezeka kwa deni la Serikali kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

Katika Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2019, nilibaini kuwa deni la Serikali limeongezeka kwa kiasi cha Sh. bilioni 16.18 kutoka Sh. bilioni 37.45 za mwaka uliopita. Nina mashaka kuwa ukwasi wa Bohari unazidi kushuka hivyo kuathiri utekelezaji wa mipango mbalimbali ikiwamo usambazaji wa dawa na vifaa tiba kwa jamii pamoja na utekelezaji wa mipango yake mbalimbali.

5.6 Hasara katika Mkataba wa Kupitisha Mawasiliano (Roaming) na Kampuni ya MIC

Shirika la TTCL liliingia mkataba na Kampuni ya MIC Tanzania kwa ajili ya kupitisha mawasiliano (roaming) yake Kitaifa kuanzia tarehe 14 Julai 2018. Dhumuni lilikuwa ni kutanua ufikaji wa mtandao nchi nzima na kuongeza mapato.

Jedwali Na. 19: Gharama za vifurushi vya kupitisha mawasiliano katika mtandao wa MIC

Kifurushi	Data	Bei anayouzia (Sh.)	Bei anayonunulia kwa MIC (Sh.)	Hasara (Sh.)
	1GB	1,500	2,500	1,000
Kwa wiki	4GB	8,000	10,000	2,000

	10GB	10,000	25,000	15,000
	15GB	30,000	37,500	7,500
Kwa mwezi	20GB	40,000	50,000	10,000
	150GB	180,000	375,000	195,000
	200GB	225,000	500,000	275,000

Nilibaini kuwa TTCL ilikuwa ikitoza bei rahisi kwenye vifurushi inavyouza kwa wateja wake kuliko bei ambayo inalipa kwa mujibu wa mkataba. Hii imesababisha TTCL ipate hasara ya Sh. bilioni 1.11 katika mkataba wa kupitisha mawasiliano pekee. Pia, kama TTCL itachukua hatua ya kuongeza bei ili kupunguza hasara, kuna uwezekano wa kupoteza mapato kutokana na ushindani mkali uliopo katika soko. Bei za huduma za kupitisha mawasiliano zinaainishwa katika **Jedwali Na. 22** hapa chini.

Jedwali Na. 20: Gharama za vifurushi vya kupitisha mawasiliano katika mtandao wa MIC

Kifurushi	Data	Bei anayouzia (Sh.)	Bei anayonunulia kwa MIC (Sh.)	Hasara (Sh.)
	1GB	1,500	2,500	1,000
Kwa wiki	4GB	8,000	10,000	2,000
	10GB	10,000	25,000	15,000
	15GB	30,000	37,500	7,500
Kwa mwezi	20GB	40,000	50,000	10,000
	150GB	180,000	375,000	195,000
	200GB	225,000	500,000	275,000

5.7 Upotevu wa Malipo yasiyo na tija kwa watumishi waliokuwa watumishi wa mashirika ya Umma fedha Sh. milioni 829.45 kwa watumishi walioacha kazi na kuhama

Nilibaini kuwa Mashirika ya Umma matatu yalilipa malipo mbalimbali yenye jumla ya Sh. milioni 829.45 kwa watumishi walioacha kazi au kuhama kwa sababu mbalimbali. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) ililipa kiasi cha Sh. milioni 398.14; Mamlaka ya Udhambi wa Mbolea Tanzania (TFRA) ililipa kiasi cha Sh. milioni 324.01. Aidha, ; na Mamlaka ya Bandari (TPA) iliripoti mikopo ya kiasi cha Sh. milioni 107.30 kama mikopo kwa iliyotolewa kwa watumishi ambao tayari wameacha waliokwisha acha kazi.

Malipo hayo ni kielelezo cha udhaifu katika usimamizi wa malipo yanayotolewa kwa watumishi na usimamizi usioridhisha wa taratibu za watumishi kuacha kazi au kuhama katika Taasisi za umma.

5.1 Malipo yasiyostahiki ya posho za likizo Sh. bilioni 1.58

Mamlaka ya Maji Safi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) ililipa kiasi cha Sh. bilioni 1.58 kama posho za mwezi wa ziada (leave passage - 13th salary leave passage) kinyume na Kanuni za Kudumu kwa watumishi wa umma na aya ya 3.1.3.13 ya Sera na Kanuni za Rasilimali Watu za DAWASA zinazotaka mtumishi kupewa posho ya kusafiri wakati wa likizo mara moja kila baada ya miaka miwili. Hali hii husababisha matumizi mabaya ya fedha za umma.

5.2 Malipo ya michango ya watumishi kwa Bima ya Afya

Nilipitia michango iliyofanywa na Shirika la Simu Tanzania (TTCL) kwenda Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa (NHIF) ambayo ilikuwa Sh. bilioni 1.075 ikiwa ni asilimia sita ya mishahara ya watumishi. Hii ni kinyume na Kifungu cha 9 cha Sheria ya Bima ya Afya Na. 9 ya mwaka 1999 kinachotaka michango igawanywe sawa sawa kati ya mwajiri na mwajiriwa. Hivyo, TTCL iliingia gharama ya ziada ya Sh. milioni 537.50 kwa kuchangia asilimia tatu alizopaswa kuchangia mwajiriwa.

Pia, DAWASA na LATRA zilichangia asilimia 6 ya mishahara wa mtumishi katika Mfuko wa Bima ya Afya ikiwa ni asilimia 3 za mwajiri na asilimia 3 za mwajiriwa na hakuna makato yaliyofanywa katika mishahara ya watumishi. Kwahiyo, mamlaka hizo ziliingia gharama ya kuchangia bima za afya zenye jumla ya Sh. milioni 690.13.

5.3 Madai ya michango na tozo za adhabu katika mifuko ya jamii Sh. bilioni 171.91

Waajiri waliosajiliwa katika mifuko ya hifadhi ya jamii wanapaswa kuwasilisha michango ya wafanyakazi wao ndani ya siku 30 za mwezi unaofuata. Tozo za adhabu hutozwa kwa waajiri wanaowasilisha michango nje ya muda uliopangwa. Hata hivyo, mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2019, nilibaini kuwa jumla ya Sh. bilioni 171.91 za michango na tozo za adhabu kutoka kwa waajiri zilikuwa hazijakusanywa katika mifuko ya NHIF, WCF na PSSSF.

Kukosekana kwa ufuatiliaji kwa wakati kunaweza kusababisha mifuko hiyo kushindwa kukusanya michango hiyo na kupelekea mifuko hiyo kupata hasara.

5.4 Shaka ya upatikanaji wa marejesho ya fedha za amana kutoka benki ya uwekezaji ya TIB Sh. bilioni 111.80

Mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2018, mifuko ya PSSSF na NHIF ilikuwa na jumla ya kiasi cha amana na riba Sh. bilioni 118.8 kilichoiva katika Benki ya Uwekezaji ya TIB. Hata hivyo nilibaini kuwa Benki ya Uwekezaji ya TIB ina

changamoto ya ukwasi ambao unapelekea Benki hiyo kushindwa kulipa amana zilizoiva kwa wakati. Mfuko wa NHIF ulikuwa na kiasi cha Sh. bilioni 16.8 na PSSF kilikuwa na Sh. bilioni 95.

Kushindwa kwa mifuko kupata kiasi kilichoiva kutoka Benki ya Uwekezaji ya TIB kunaathiri uwezo wa kifedha wa mifuko hiyo.

5.5 Kutokuwa na uhakika wa urejeshwaji wa mkopo kwa watumishi waliondoka katika mfuko wa NHIF Sh. milioni 974.20

Nilibaini Mfuko wa NHIF unadai mkopo kwa watumishi walioacha kazi kiasi cha Sh. milioni 974.20 mpaka tarehe 30 Juni, 2019. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 744 ukilinganisha na Sh. milioni 115.47 mkopo kwa watumishi walioacha kazi katika kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2018. Aidha, nilibaini wafanyakazi hao hawafanyi marejesho ya mikopo yao na hakuna makubaliano yoyote ya namna ya kurejesha mikopo hiyo kati ya Mfuko na wafanyakazi hao. Hali hii inaleta shaka juu ya urejeshwaji wa mkopo kwa wafanyakazi hao.

5.6 Deni la Serikali kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Bima ya Afya Sh. trilioni 2.42

Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii na Bima ya Afya ina madai makubwa ambayo ni chechefu, mengi ya madeni hayo ni kwa Serikali na taasisi zake. Mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2019, mifuko hiyo ilikuwa inaidai Serikali pamoja na Taasisi zake kiasi cha Sh. trilioni 2.42 kama ifuatavyo:

Jedwali Na.21: Madeni ya Serikali kwa Mifuko ya Hifadhi ya jamii na Bima ya Afya kwa mwaka 2019

Jina la Mfuko	Kiasi
NSSF	Trilioni 1.47
PSSF	Bilioni 731.40
NHIF	Bilioni 220.39
Jumla	Trilioni 2.42

5.7 Hasara inayotokana na Maji Yanayopotea Sh. bilioni 155.84

Ukaguzi ulibaini upotevu wa maji katika Mamlaka za maji bado ni mkubwa ukilinganisha na asilimia 20 inayokubalika. Katika ukaguzi uliofanyika kwa Mamlaka za Maji 20 kuhusu upotevu wa maji, nilibaini Mamlaka Moja tu ya Kahama ndiyo ilikuwa na asilimia inayokubalika kwenye upotevu wa maji.

Mamlaka 19 zilizobaki ziliendelea kupata hasara kubwa ya upotevu wa maji kwa zaidi ya kiwango cha uhimilivu cha upotevu wa maji. Kiasi cha upotevu kwa mamlaka zote hizi kilikuwa Sh. bilioni 155.84 ambacho ni zaidi ya kiwango cha uvumilivu wa upotevu ambacho ni Sh. bilioni 74.14. Hii ina maana kwamba

tofauti ya Sh. bilioni 81.70 zilikuwa katika kiwango kisichovumilika cha upotevu kulingana na taarifa zilizopo za kiwango cha maji kinachozalishwa na idadi ya wateja waliounganishwa.

5.8 Ucheleweshwaji wa makusanyo ya madeni katika Mamlaka za Maji Sh. bilioni 106.31

Nilibaini kiwango cha chini cha urejeshaji wa madeni katika Mamlaka za Maji kwani idadi kubwa ya mapato hayajarejeshwa na yalikuwa yamezidi muda uliowekwa kwenye sera ya mikopo inayotaka kumuondolea mteja huduma ya maji asipolipa kwa zaidi ya siku 90.

Katika mkusanyiko huo wa madeni, nilibaini kuwa kati ya Sh. bilioni 106.31, Sh. bilioni 35.08 (sawa na asilimia 33) ni madeni ya Serikali; na Sh. bilioni 71.23 (sawa na asilimia 67) ni madeni kutoka kwa wateja wengine. Ongezeko la madeni husababishwa na kutokuwa na ufuatiliaji wa karibu wa ukusanyaji wa wadeni.

5.9 Malipo ya tozo za adhabu za kiasi cha Sh. milioni 912.97 kutokana na ucheleweshaji wa malipo

Ukaguzi wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Maji (MAJI HOUSE) katika eneo la Ubungo-Dar-es-Salaam lenye thamani ya Sh. Bilioni 44 ulibaini malipo ya kiasi cha Sh. milioni 912.97 yaliyofanywa kwa mkandarasi kama tozo za adhabu ya kuchelewesha malipo. DAWASA ililipa kiasi cha Sh. milioni 472.26 cha tozo hiyo na kiasi kilichobakia cha Sh. milioni 440.71 kililipwa na Wizara ya Maji.

5.10 Madai yaliyokosa uthibitisho Sh. bilioni 291.17

Wakati wa uhakiki wa madeni ya Shirika la Uzalishaji Umeme Tanzania (TANESCO) niliomba uthibitisho wa madeni ya toka kwa wadeni, ambapo ni kampuni 23 pekee ndizo zilizoweza kuthibitisha madeni yao yenye thamani ya Sh. bilioni 647.33 huku kampuni 913 zenye madai yenye thamani ya Sh. bilioni 291.17 hazikuweza kuthibitisha madai yao, kati yao ipo kampuni ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL) yenye jumla ya madai ya Sh. bilioni 102.12, kampuni hii ilishindwa kufanya uthibitisho wa deni lake kutokana na changamoto za kiutendaji zinazoikabili kampuni.

SURA YA SITA
MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

Ndugu Waandishi wa habari,

Ukaguzi wangu wa miradi ya maendeleo umebaini yafuatayo:

6.1 Malipo ya Sh. bilioni 6.51 yaliyofanyika bila uthibitisho wa stakabadhi za kielektroniki

Nilibaini malipo yenye kiasi cha Sh. bilioni 6.51 kwenye miradi 58 ambayo hayakuambatanishwa na stakabadhi za kielektroniki kinyume na Kanuni ya 28 (1) ya Kodi ya Mapato (Vifaa vya Mfumo wa Kielektroniki) ya mwaka 2012. Kutokudai stakabadhi za kielektroniki kunapunguza jitihada za Serikali za kukusanya kodi na vile vile kunasaidia ukwepaji wa kodi.

6.2 Kodi ya zuio ya Sh. bilioni 3.86 haikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania

Nilibaini kiasi cha Sh. bilioni 3.86 kilichozuiwa kutoka kwenye malipo yaliyofanywa kwa wazabuni wa bidhaa na huduma hakikuwasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

6.3 Fidia ya Sh. bilioni 5.82 kwa watu walioathiriwa na miradi hazijalipwa

Mapitio ya usimamizi wa miradi yamebaini kuwa fedha za fidia kiasi cha Sh. bilioni 5.82 hazikulipwa kwa watu walioathirika na utekelezaji wa miradi ya Programu ya Uboreshaji wa Miundombinu ya Usafirishaji Jijini Dar es salaam (DUTP) na Programu ya Kusaidia Sekta Ya Usafirishaji (TSSP).

6.4 Bakaa ya Sh. bilioni 1.63 hazijarejeshwa kwenye akaunti zinazotunza fedha za washirika (Holding Accounts)

Nilibaini kuwa Sh. bilioni 1.63 ikiwa ni bakaa ya fedha za mradi wa Mfuko Mkuu wa Fedha za Afya hazijarejeshwa kwenye Akaunti zinazotunza fedha za Washirika (Holding Accounts) kwa muda wa miaka mitatu kutokana na maombi ya kuhamisha fedha hizo kuchelewa kupelekwa Wizara ya Fedha na Mipango.

Kuchelewa kurejeshwa kwa bakaa ya fedha kwenye Akaunti zinazotunza fedha za washirika kunaweza kuathiri mapokezi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.

6.5 Malipo yasiyokubalika Sh. bilioni 2.9

Katika mwaka wa ukaguzi, nilibaini watekeleza miradi 20 walifanya malipo yasiyokubalika kiasi cha Sh. bilioni 2.90 ambayo ni kinyume na matakwa ya mkataba.

6.6 Fedha za miradi zilizokopwa bila kurejeshwa Sh. milioni 972.82

Nimebaini kwamba Maafisa Masuuli kwenye miradi saba walikopa fedha za miradi kiasi cha Sh. milioni 972.82 ili kugharamia matumizi mbalimbali ya kawaida bila kurejesha fedha hizo kwenye miradi husika.

6.7 Uwepo wa bakaa dola za Kimarekani milioni 25.16 kwa muda mrefu kwenye akaunti zinazotunza fedha za washirika

Mapitio yangu ya akaunti zinazotunza fedha za washirika zilizopo Wizara ya Fedha na Mipango umebaini kuwepo kwa bakaa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 25.16 zinazohusiana na miradi 12 ambapo mingi ya miradi hiyo tayari imeshafungwa na fedha zimeendelea kubaki kwenye Akaunti hizo kwa muda hadi miaka saba.

SURA YA SABA

MATOKEO YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

Ndugu Waandishi wa habari,

Nimekagua mifumo mbalimbali ya TEHAMA katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2019. Ufuatao ni muhtasari wa mambo yaliyojitokeza kwenye ukaguzi huo.

7.1 Uratibu hafifu wa kuunganisha mifumo ya TEHAMA

Nilibaini mapungufu katika kutambua, kuratibu na kushughulikia juhudi zinazofanana katika kubuni mifumo ya TEHAMA kwenye Taasisi za umma. Hii inapelekea ugumu kwenye uunganishwaji wa mifumo hii.

7.2 Mapungufu katika mfumo wa kufuatilia magari wa LATRA

Ukaguzi wa Mfumo wa kudhibiti mwendokasi wa magari unaotumiwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), ulibaini kuwa utayarishaji wa gharama za adhabu kwa makosa yaliyofanyika hufanywa na maafisa nje ya mfumo baada ya kupokea ripoti kutoka kituo cha udhibiti.

Kitendo hiki kinaweza kupelekea makosa ya kibinadamu na udanganyifu sababu uamuzi upo chini ya maafisa wa LATRA kuamua ni kiasi gani kinachopaswa kulipwa kwa makosa yaliyobainika.

Pia, nimebaini kutokuwepo kwa taarifa za usuluhishi baina ya makosa yaliyotendeka na kiasi kilicholipwa. Vilevile, hakuna njia za kufuatilia malipo yasiyolipwa kwa namba za udhibiti za malipo “control number” zilizopitwa na wakati. Mfano, nilibaini taarifa ya kiasi cha Sh. milioni 185.67 katika baadhi ya Ofisi za mikoa ambapo namba za udhibiti zimepitwa na wakati kabla ya malipo kufanyika.

7.3 Mapungufu katika mfumo wa kielektroniki wa malipo ya Serikali (GePG)

Ukaguzi wangu katika Idara ya Uhamiaji umebaini mfumo wa mfumo wa kielektroniki wa malipo ya Serikali (GePG) unakubali kadi za VISA na MasterCard pekee kwa malipo ya mtandao. Lakini haukubali malipo ya kadi nyingine kama PayPal, Maestro, eBay, Cirrus, American Express na Delta. Hii inapelekea usumbufu kwa baadhi ya wateja na huenda ikapelekea ukosefu wa mapato.

Pia, nimebaini changamoto wanayoipata Watanzania wanaoishi nje ya nchi wanapolipia hati zao za kusafiria ambazo hugharimu Dola 75 za Kimarekani

kama ada ya huduma. Malipo haya hukataa kwa baadhi ya nchi ambazo benki patanishi hukata kiasi cha Dola 10 za Kimarekani kama ada ya muamala, hivyo kupelekea bakaa ya Dola 65 za Kimarekani na kusababisha malipo kukataliwa na mfumo wa malipo wa GePG kwasababu ni pungufu ya ada ya huduma ambayo ni Dola 75 za Kimarekani.

Pia, katika ukaguzi wa TANAPA nimebaini baadhi ya namba za udhibiti hulipwa mara mbili kwa malipo ya njia ya mtandao kupitia mfumo wa GePG. Kwa kawaida malipo ya GePG kwa njia ya mtandao huchukua muda wa masaa 24 kupokelewa katika mfumo wa mapato wa TANAPA. Hii husababisha namba ya malipo ionekane haijalipiwa na kumuwezesha mlipaji kulipa tena kwa njia nyingine.

Ni maoni yangu kuwa suala hili huenda likasababisha usumbufu kwa TANAPA ambapo hutakiwa kutambua na kurudisha malipo ya ziada kwa wateja, kusababisha makosa katika taarifa za hesabu za mamlaka, au vyote kwa pamoja.

7.4 Kuwa na Mifumo tofauti inayofanya Kazi Moja

Katika ukaguzi wa miradi ya mifumo ya TEHAMA nimebaini mwaka 2018 Bodi ya Sukari ya Tanzania (SBT) iliboresha mifumo yake miwili; Mfumo wa uingizaji sukari na mfumo wa usajili wa wakulima wa miwa. Lakini nimebaini kuwa Wizara ya Kilimo ilikuwa na miradi ya kuunda mifumo kama hiyo kwa Mawakala wake wote. Hivyo SBT italazimika kuanza kutumia mifumo ya Wizara na kuacha mifumo yake iliyoboreshwa licha ya gharama iliyoingiwa. Suala hili limeingiza Serikali gharama ambazo zingeweza kuepukika endapo kungekua na uratibu mzuri baina ya Wizara mama na Taasisi zake kuhusu miradi ya vipaumbele.

7.5 Ucheleweshaji wa ununuzi wa mfumo wa mtandao wa kufuatilia kesi za Baraza la Ushindani

Ukaguzi wangu wa Baraza la Ushindani Tanzania (FCT) ulibaini kuwepo kwa mpango wa kununua vifaa vya kurekodi taarifa wakati wa vikao vya kesi na kununua mfumo wa TEHAMA wa kufuatilia muendelezo na hali za kesi ili kuongeza ufanisi katika usikilizaji wa kesi. Hata hivyo, ununuzi wa mfumo huo haukufanyika licha ya kuwepo safari kadhaa za ziara za mafunzo zilizofanywa na maafisa wa Baraza nchini Canada na Afrika Kusini ambazo ziligharimu jumla ya Sh. milioni 42.37 na Dola za Kimarekani 140,215.

Ni maoni yangu kuwa suala hili limesababishwa na upungufu katika usimamizi na ukosefu wa vipaumbele katika kutekeleza ununuzi wa mfumo tajwa.

SURA YA NANE

MATOKEO YA KAGUZI MAALUMU

Ndugu Waandishi wa habari,

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2019 nilifanya ukaguzi maalum kwa taasisi mbalimbali za Serikali za Mitaa, Serikali kuu, na Mashirika ya Umma. Nilikamilisha jumla ya kaguzi 20 za ukaguzi maalumu. Mambo yaliyojitokeza kwenye kaguzi hizo yameelezwa kwa muhtasari kwenye ripoti zangu.

SURA YA TISA

MATOKEO YA UKAGUZI WA UFANISI

Ndugu Waandishi wa habari,

Sura hii inaeleza kwa ufupi mapungufu yaliyobainika katika Ripoti tano za Ukaguzi wa Ufanisi katika sekta ya maji zilizofanyika mwaka 2016 na 2019 zinazohusu usimamizi wa mikataba ya ujenzi wa miradi ya maji mijini, uhibitaji wa uvunaji wa maji kutoka kwenye vyanzo vya maji, usimamizi wa utoaji wa huduma za maji taka maeneo ya mijini, miradi ya usambazaji wa maji yatokanayo na visima virefu na usimamizi wa miradi ya maji vijijini.

9.1 Matokeo ya kaguzi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:

- Ilibainika kwamba kufikia mwaka 2017/18 huduma za maji safi na salama zilikuwa zimefikia asilimia 58.7 tu ya idadi ya watu wanaoishi vijijini.
- Ukaguzi pia ulibaini kuwa asilimia 91 ya wakazi wa mijini hawapati huduma za maji taka.
- Ukaguzi ulibaini kuwa usimamizi wa mikataba ya miradi ya maji haukufanyika ipasavyo. Baadhi ya wakandarasi wasiokuwa na sifa na uwezo wa kutekeleza miradi kulingana na matakwa ya mikataba walipewa kazi za kutekeleza miradi hiyo.
- Kulikuwapo kwa gharama kubwa za kuchimba visima ambazo zilikuwa juu ya wastani wa gharama ya kuchimba visima kwa kila mita. Miradi ilitekelezwa kwa gharama kubwa kuliko gharama zilizokubaliwa awali. Ongezeko la bei kwa miradi yote ilikuwa karibu Sh. bilioni 30, ambayo ni sawa na asilimia 28 ya bei ya awali ya mikataba.

9.2 Masuala yaliyoonekana katika taarifa 12 za Ukaguzi wa Ufanisi uliofanyika mwaka huu:

9.2.1 Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Upatikaniaji wa Umeme na Uhakika wa Utaoji Huduma za Umeme

- TANESCO ilikuwa na wateja 72,463 ambao hawajafanyiwa upimaji kwa ajili ya kuunganishiwa huduma na wateja 155,127 ambao walishalipia gharama ila hawajaunganishiwa umeme. Ucheleweshaji huu umelipotezea Shirika mapato yaliyokadiriwa kufikia Sh. bilioni 60.7 kupitia malipo ya kuunganishwa. Na kiasi cha Sh. bilioni 8.33 kupitia matumizi ya umeme.

- TANESCO ilipoteza wastani wa kiasi cha Sh. bilioni 67 kwa mwaka kutokana na upotevu wa nishati ya umeme.

9.2.2 Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Ukusanyaji Mapato toka vyanzo vya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

- Kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2018/19, takribani 70% ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikufikia malengo yao ya ukusanyaji wa mapato.

Baadhi ya mapungufu yaliyoonekana katika mfumo wa ukusanyaji mapato ni:

- Maafisa wa Halmashauri kutokuwa na uwezo na uelewa wa kutosha wa kutumia vizuri mfumo wa Serikali za Mitaa wa ukusanyaji mapato na mashine za kukusanyia mapato.
- Mashine za kukusanyia mapato (POS) mara nyingi hazikuunganishwa kwenye mtandao na hivyo kufanya mapato yaliyokusanywa kutoonekana katika mfumo wa mapato ya Halmashauri husika.
- Tarehe katika POS kadhaa kurudhishwa nyuma na hivyo kufanya mapato husika kutoonekana katika orodha ya mapato ya siku husika.

9.2.3 Ukaguzi wa Ufanisi katika utekelezaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Kupambana na Utakatishaji wa Fedha haramu

- Ukaguzi ulibaini kuwa hapakuwa na Sera ya kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu nchini.
- Ukaguzi ulibaini mapungufu kwenye kuzingatia mahitaji ya kisheria ya kupambana na utakatishaji wa fedha haramu hasa katika utoaji wa taarifa za miamala shuku yenye viashiria vya utakatishaji wa fedha. Hii ilichangiwa na udhaifu katika kutoa taarifa za miamala shuku kwa wakati na katika mfumo sahihi na kutokuwepo kwa miongozo ya kisékta.

9.2.4 Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Shughuli za Manunuzi ya Umma

- Ukaguzi umebaini kwamba, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilitumia njia ya manunuzi isiyo na ushindani “single source” kwenye manunuzi yenye thamani ya Sh. bilioni 22.69 bila sababu za msingi.
- Wakala wa Ununuzi wa Mafuta ya Jumla ulifanya kazi za manunuzi yenye thamani ya Sh. milioni 3.28 bila kuwa na Bodi ya Zabuni wala Kitengo cha Manunuzi.

9.2.5 Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Shughuli za Kinga na Chanjo

- Kulikuwa na ucheleweshwaji wa usambazaji wa chanjo na vifaa tiba vya chanjo za Surua, Kupooza, Kuharisha, Dondakoo, Kifaduro, Pepopunda, Homa ya Ini na Kichomi ambao ulifikia hadi siku 61. Hali hii ilichangia ukosefu wa chanjo kwenye baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya.
- Kuanzia mwaka 2017 hadi 2019, Wizara ya Afya haikutekeleza shughuli zote za kinga na chanjo kama ilivyopanga. Ukaguzi ulibaini kuwa shughuli 13 za chanjo hazikuwa zimetetelezwa.

9.2.6 Ukaguzi wa Ufanisi katika Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa ya Mifugo

- Ukaguzi ulibaini ucheleweshaji katika kubaini na kuwasilisha taarifa za magonjwa ya wanyama na mfumo hafifu wa uthibitisho wa maabara inayosababishwa na maabara kufikiwa na wafugaji wa mjini tu hasa wale waliokaribu na ofisi za kanda.
- Ukaguzi ulibaini kiwango cha uchanjaji wa mifugo kilikuwa chini ya asilimia 10 na kwa mwaka 2016 na 2017 uchanjaji wa mifugo ulikuwa chini ya asilimia moja.
- Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Mifugo haikufanya ufuatiliaji wowote kwa mwaka wa fedha 2016/17 na 2017/18 kwa sababu hakukuwa na fedha iliyotengwa kwa shughuli hiyo kwa miaka iliyotajwa.

9.2.7 Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Upatikanaji usioridhisha wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

- Ukaguzi umebaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilishindwa kufikia lengo la kudahili wanafunzi 1,012,967 wa elimu ya ufundi stadi hadi mwaka 2017/18 ambapo ilifanikiwa kudahili wanafunzi 119,184 tu hivyo kuwa na upungufu wa wanafunzi 893,783.
- Ukaguzi ulibaini kuwa vyuo vilivyotembelewa vilikuwa na asilimia 57 tu ya zana na vifaa vya kufundishia vilivyohitajika. Pamoja na hayo zana na vifaa vya kufundishia vilivyopo kwenye vyuo hivyo vilikuwa vimepitwa na wakati na vilikuwa chakavu.

SURA YA KUMI

HITIMISHO

Ndugu Waandishi wa habari,

Masuala niliyowasilisha hapa ni muhtasari wa mambo machache niliyoyaona ni muhimu zaidi kuwafahamisha. Hata hivyo, Ripoti zilizokabidhiwa bungeni zina mambo mengi zaidi na mapendekezo kwa kila suala kwa lengo la kuongeza uwajibikaji na usimamizi wa rasilimali za umma. Ni matumaini yangu kwamba mtapata muda wa kuzisoma ili muweze kuuhabarisha umma mambo mbalimbali yanayohusu ukaguzi uliofanyika.

Ndugu Waandishi wa habari,

Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa kunisikiliza na nawatakia kazi njema.

Mungu awabariki.

Asante Sana.

Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**